



EAST AFRICAN COMMUNITY

**KANUNI ZA UMOJA WA
FORODHA YA JUMUIYA YA
AFRIKA MASHARIKI
(KANUNI ZA ASILI) ZA 2015**

TOLEO LA KISWAHILI



EAST AFRICAN COMMUNITY

KANUNI ZA UMOJA WA FORODHA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI (KANUNI ZA ASILI) ZA 2015

TOLEO LA KISWAHILI

KANUSHO

Kitini hiki kimeweza kuandaliwa kwa msaada wa ukarimu kutoka kwa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Marekani (USAID). Yaliyomo kwenye kitini hiki yameandaliwa na Kituo cha kikanda cha Utafiti wa Maendeleo Jumuishi (RCID Ltd) na hayalazimiki kuwa ni maoni ya USAID au Serikali ya Marekani.



Kanuni za Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Kanani za Asili) za 2015
Arusha, Tanzania

ISBN 978-9987-786-07-7

**KANUNI ZA UMOJA WA FORODHA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI
(KANUNI ZA ASILI) ZA 2015**

YALIYOMO

KICHWA CHA SHERIA

KANUNI ya 1:	Dondoo
KANUNI ya 2:	Azma ya Kanuni za Asili
KANUNI ya 3:	Tafsiri
KANUNI ya 4:	Vigezo vya Asili
KANUNI ya 5:	Bidhaa zilizotolewa kwa Ujumla katika Nchi Mbia
KANUNI ya 6:	Bidhaa zilizotengenezwa kwa kutumia vifaa visivyotoka kwa Nchi Mbia
KANUNI ya 7:	Taratatibu zisizotekeleza mashauriano kuhusu Chimbuko
KANUNI ya 8:	Mkusanyiko wa Asili
KANUNI ya 9:	Kitengo cha kufuzu
KANUNI ya 10:	Mikusanyiko
KANUNI ya 11:	Utengo wa Vifaa
KANUNI ya 12	Matayarisho ya Michanganyiko
KANUNI ya 13	Matayarisho ya Upakiaji
KANUNI ya 14	Vipengele visivyohusika
KANUNI ya 15	Eneo
KANUNI ya 16	Usafiri wa moja kwa moja
KANUNI ya 17	Utoaji wa Cheti cha Asili
KANUNI ya 18	Kutolewa kwa nakala ya Cheti cha Asili
KANUNI ya 19	Kutolewa kwa Cheti cha Asili kwa misingi ya ithibati ya asili ilitoyotolewa au kutengenezwa hapo awali
KANUNI ya 20	Msafirishaji bidhaa nje aliyeidhinishwa
KANUNI ya 21	Uhalali wa ithibati ya asili
KANUNI ya 22	Kusamehewa kutoka kwa Cheti cha Asili

KANUNI ya 23	Taarifa ya habari kuhusu mamlaka zenye ustadi
KANUNI ya 24	Uthibitishaji wa ithibati ya asili
KANUNI ya 25	Uhifadhi wa hati
KANUNI ya 26	Ukiukaji na adhabu
KANUNI ya 27	Mwongozo
KANUNI ya 28	Maagizo kutoka kwa Baraza
KANUNI ya 29	Kikomo cha Kanuni za Asili
KANUNI ya 30	Kubatilishwa kwa Kanuni za Jumuiya ya Afrika Mashariki (Kanuni za Asili)

RATIBA: ANDIKO

Ratiba ya Kwanza	Orodha ya bidhaa na kazi au shughuli za usindikaji zinazojadili asili
Ratiba ya Pili	Vyeti vya Asili vya Jumuiya ya Afrika Mashariki
Ratiba ya Tatu	Tamko la Wauzaji/Watengenezaji bidhaa
Ratiba ya Nne	Tamko la Asili
Ratiba ya Tano	Fomu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya uthibitishaji wa asili
Ratiba ya Sita	Cheti cha habari cha Jumuiya ya Afrika Mashariki

**KANUNI ZA UMOJA WA FORODHA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI
(KANUNI ZA ASILI) ZA 2015**

KANUNI YA KWANZA

Dondoo

Kanuni hizi zinaweza kutajwa kama Kanuni za Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Kanuni za Asili) 2015.

KANUNI YA PILI

Azma ya Kanuni za Asili

Azma ya kanuni hizi ni kutekeleza masharti ya Makala ya 14 ya Itifaki na kuhakikisha kuwa kuna usawa kati ya nchi mbia katika ufuataji wa Kanuni za Asili na kwa kiasi fulani kuwezesha mchakato kuwa na uwazi, wenye kuwajibika na wa haki; wenye kutabirika na sambamba na masharti ya Itifaki hiyo.

KANUNI YA TATU

Tafsiri

Katika kanuni hizi, isipokuwa iwapo muktadha utakanusha:

“**Mkutano**” inamaanisha mchakato wa utengenezaji unaotumia miundo sahihi, ulio na mpangilio na vifaa maalumu;

“**Imeainishwa**” inamaanisha uainishaji wa bidhaa chini ya kichwa au kichwa kidogo katika Maelezo ya Bidhaa yaliyounganishwa na mfumo maalum wa usimbuaji;

“**Kamati**” inamaanisha Kamati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inayohusika na tiba za biashara zilizoanzishwa chini ya Makala Nambari 24 ya Itifaki ya Uanzishaji wa Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

“**Mamlaka yenye uwezo**” inamaanisha shirika lililoteuliwa na nchi mbia kutoa cheti cha chimbuko;

“**kugongwa chini kabisa**” inamaanisha kifurushi kilicho na sehemu na vijishehemu vidogo vidogo vinavyotumika katika kutengeneza bidhaa zilizokamilika;

“**Baraza**” inamaanisha baraza la mawaziri wa Jumuiya lililoanzishwa kupitia Makala Nambari 9 ya Mkataba;

“**Thamani ya Forodha**” inamaanisha thamani kama ilivyodhamiriwa kwa mujibu wa Sehemu ya 122 ya Sheria za Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2004;

“**Bei ya kazi za zamani**” inamaanisha bei aliyoamuliwa kulingana na masharti ya Ratiba ya Kwanza iliyolipwa kwa bidhaa za kazi za zamani kwa mtengenezaji katika nchi mbia ambayo kwayo, kazi ya mwisho au usindikaji unatekelezwa;

“**Nchi ya kigeni**” inamaanisha nchi nyingine isiyo moja ya nchi mbia;

“**Kanuni za Uhasibu zinazokubalika kwa ujumla**” inamaanisha makubaliano yanayotambuliwa au msaada mkubwa wa mamlaka unaotolewa kwa eneo la nchi mbia kwa minajili ya kurekodi mapato, gharama, mali na madeni, utoaji wa taarifa na utayarishaji wa taarifa za kifedha. Kanuni za Uhasibu zinazokubalika kwa Ujumla zinaweza kujumlisha mwongozo kwa kina kwa matumizi ya ujumla pia viwango vya kina, mazoea na taratibu;

“**Bidhaa**” inamaanisha vifaa na bidhaa;

“**Kichwa**” inamaanisha misimbo iliyo na tarakimu nne inayotumika katika Maelezo ya Bidhaa na mfumo wa kuweka alama;

“**Bahari Kuu**” ina maana moja na Mapatano ya Umoja wa Mataifa kuhusu Sheria za Baharini;

“**Utengenezaji**” ni usindikaji wowote unaohitaji uwekezaji wa kiteknologia, miundombinu na nguvukazi ambavyo kwavyo, bidhaa mwishowe hutengenezwa.

“**Vifaa**” ni malighafi, bidhaa zilizopangwa, bidhaa kamilifu, viungo, sehemu na vifaa vinavyotumika katika utengenezaji wa bidhaa;

“**Kiwango cha juu cha vifaa visivyo vya asili**” inamaanisha kiwango cha juu vifaa visivyo vya asili vinavyoruhusiwa ili kutambua utengenezaji unaofanya kazi au usindikaji ulio wa kutosha kutunukiwa hali asilia ya bidhaa. Hii inaweza kuonyeshwa kama asilimia ya bei ya kazi za zamani za bidhaa au kama asilimia ya uzito wavu wa vifaa hivi vilivyotumika vilivyo chini ya kundi maalum la aya, kichwa au kichwa kidogo;

“**Vifaa visivyo vya asili**” ni vifaa vinavyotoka nje ya nchi mbia;

“**Sehemu**” hii ni sehemu binafsi, ilivyooundwa au kutengenezwa kutokana na chuma au kifaa kingine pekee, ambacho hakikuunganishwa kwa njia yeyote na sehemu au kifaa kingine;

“**Nchi Mbia**” inamaanisha Jamhuri ya Burundi, Jamhuri ya Kenya, Jamhuri ya Rwanda, Jamhuri ya Tanzania, Jamhuri ya Uganda na nchi nyingine yeyote iliyopewa nafasi ya uanachama katika Jumuiya chini ya Kifungu cha Tatu cha Mkataba huo;

“**Zilizotengenezwa**” na “**Mchakato wa Utengenezaji**” ni jumla ya utendaji wa kazi yeyote au michakato kama ilivyotolewa katika Kanuni ya saba ya Kanuni hizi;

“**Mtengezaji/Mzalishaji**” inajumuisha, kati ya vingine, uchimbaji madini, utengenezaji bidhaa au biashara ya kilimo au mkulima yeyote binafsi au fundistadi anayesambaza bidhaa kwa ajili ya kuuza nchi za nje;

“**Bidhaa**” ni bidhaa iliyotengenezwa, ikiwamo bidhaa iliyokusudiwa kwa matumizi ya baadaye katika kazi nyingine ya utengenezaji wa bidhaa;

“**Itifaki**” ni Itifaki au protokali inayopatikana katika Jumuiya ya Forodha ya Afrika Mashariki;

“**Sekretarieti**” ni Kamati/Sekretarieti ya Jumuiya iliyoanzishwa kupitia Kifungu cha tisa cha Mkataba huo;

“**Kichwa Kidogo**” ni misimbo ya tarakimu sita inayotumika katika Maelezo ya Bidha Yaliounganishwa pamoja na mfumo wa kuweka alama;

“**Mkutano wa Kilele**” Ni Mkutano wa Juu ulioanzishwa kupitia Kifungu cha tisa cha Mkataba huo;

“**Msambazaji**” ni mtu wa kiasili au wa halali anayesambaza bidhaa kwa ajili ya kutengenezwa zaidi ndani ya Nchi Mbia au kwa usambazaji kwa Nchi Mbia nyingine;

“**Eneo**” inajumuisha “eneo bahari” na “ukanda wa kipekee wa kiuchumi” za Nchi Mbia kama ilivyofafanuliwa katika Mapatano ya Umoja wa Mataifa kuhusu Kanuni za Bahari;

“**Mkataba**” ni Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;

“**Thamani ya Vifaa visivyo vya asili**” iliyo katika orodha ya Sehemu ya kwanza ya Ratiba ya Kwanza inamaanisha thamani ya forodha wakati wa uagizaji wa vifaa visivyo vya asili vilivyotumiwa, au, endapo hii haijulikani na haiwezi kuhakikishwa, basi bei ya kwanza inayoweza kuhakikishwa kulipiwa vifaa hivyo kwa Nchi Mbia;

“**Thamani Iliyoongezwa**” ni bei ya kazi za zamani za bidhaa ya mwisho kasoro thamani ya forodha ya vifaa vilivyoagizwa kutoka nje ya Nchi Mbia na kutumika katika mchakato wa utengenezaji;

“**Chombo cha Nchi Mbia**” ni chombo cha majini cha Nchi Mbia kilichosalijiwa au kinachopeperusha bendera ya Nchi Mbia na kukidhi masharti yafuatayo:

(a) Angalau asilimia ishirini (20%) ya maafisa wa chombo hicho ni wananchi wa Nchi Mbia;

(b) Angalau asilimia ishirini (20%) ya wafanyakazi ni wananchi wa Nchi Mbia; au

(c) Angalau asilimia ishirini (20%) inayoshikilia usawa kwenye chombo inashikiliwa na wananchi wa Nchi Mbia au taasisi, wakala, biashara au shirika la serikali za Nchi Mbia.

KANUNI YA NNE

Vigezo vya Asili

1. Bidhaa zitakubalika kuwa za asili katika Nchi Mbia iwapo bidhaa -
 - (a) zimetengenezwa kiujumla katika Nchi Mbia kama ilivyotolewa katika Kanuni ya tano; au
 - (b) zimetengenezwa katika Nchi Mbia kutumia vifaa ambavyo havikupatikana humo, mradi vifaa hivyo vimefanyiwa kazi au usindikaji katika Nchi Mbia kama ilivyotolewa katika Kanuni ya sita.
2. Kwa ajili ya kutekeleza kanuni hizi, Nchi Mbia zitachukuliwa kuwa eneo moja.

KANUNI YA TANO

Bidhaa zilizotengenezwa kwa ujumla katika Nchi Mbia

1. Kwa ajili ya Kanuni ya Nne 4 (a), bidhaa zifuatazo zitachukuliwa kuwa bidhaa zilizotengenezwa kwa ujumla katika Nchi Mbia:
 - (a) madini yaliyochimbwa kutoka kwa ardhi au katika bahari ya Nchi Mbia;
 - (b) bidhaa za mboga zikiwemo mimea na bidhaa za mimea zilizovunwa, kukusanywa au kuchukuliwa kutoka kwa Nchi Mbia;
 - (c) wanyama walio hai waliozaliwa na kufugwa ndani ya mipaka ya Nchi Mbia;
 - (d) bidhaa zilizopatikana kutoka wanyama walio hai katika Nchi Mbia;
 - (e) bidhaa zilizotoka kwa wanyama waliochinjwa; waliozaliwa na kufugwa ndani ya Nchi Mbia;
 - (f) bidhaa zilizopatikana kupitia uwindaji au uvuvi ndani ya Nchi Mbia;
 - (g) bidhaa/Mazao ya ukulima wa majini, ikiwamo ukulima wa samaki na viumbe vingine vya majini, vilivyopatikana ndani ya Nchi Mbia ambamo samaki walizaliwa na kufugwa;
 - (h) bidhaa za ukulima wa baharini na bidhaa nyingine zilizochukuliwa kutoka eneo la kipekee la kiuchumi la Nchi Mbia;
 - (i) bidhaa za uvuvi wa baharini na bidhaa nyingine zilizochukuliwa kutoka maji ya bahari kuu kwa chombo cha Nchi Mbia;

- (j) bidhaa zilizotengenezwa katika kiwanda meli ya Nchi Mbia pekee kutoka kwa bidhaa zilizotajwa katika kifungu cha (i);
 - (k) bidhaa zilizotolewa kutoka kwa udongo wa baharini au udongo wa bahari iliyo nje ya maeneo ya Nchi Mbia mradi Nchi Mbia hiyo ina haki ya kufanya kazi katika udongo huo;
 - (l) vitu vilivyotumika vinavyoweza kutumika kwa kujipatia vifaa, mradi vitu hivyo vikusanywe kutoka kwa watumiaji ndani ya Nchi Mbia;
 - (m) chakavu na taka zinazotokana na shughuli za utengenezaji ndani ya Nchi Mbia; na
 - (n) bidhaa zilizotengenezwa ndani ya Nchi Mbia pekee au aghalabu kutoka –
 - i. bidhaa zilizotajwa katika kifungu hiki; na
 - ii. vifaa visivyokuwa na vitu vilivyoletwa kutoka nje ya Nchi Mbia au vilivyo na asili isiyojulikana.
2. Katika kuamua:
- (a) mahali pa utengenezaji wa bidhaa za baharini kuhusiana na Nchi Mbia, chombo cha Nchi Mbia kitachukuliwa kama sehemu ya eneo la hiyo Nchi Mbia; na
 - (b) asili ya bidhaa, bidhaa za baharini zilizochukuliwa kutoka bahari kuu au bidhaa zilizotoka baharini zitachukuliwa kuwa asili yake ni eneo la Nchi Mbia zilikopelekwa na chombo, au pia, bidhaa zilizotengenezwa ndani ya chombo cha hiyo Nchi Mbia na kuletwa moja kwa moja hadi kwenye maeneo ya hizo Nchi Mbia.

KANUNI YA SITA

Bidhaa zilizotengenezwa kutumia Vifaa visivyotoka katika Nchi Mbia

1. Kwa ajili ya Kanuni ya Nne 4(b), bidhaa itachukuliwa kufanyiwa kazi ya kutosha au kusindikwa kikamilifu endapo bidhaa iliyotajwa katika safu ya pili ya Sehemu ya Kwanza ya Ratiba ya Kwanza itakuwa sambamba na vigezo vya asili katika safu ya tatu.
2. Uamuzi kuhusu iwapo mahitaji ya Sehemu ya Kwanza ya Ratiba ya Kwanza yatakuwa yametimizwa, utafanywa kwa kila bidhaa
3. Iwapo bidhaa ambayo imeshajulikana hali asili yake kwa kutimiza vigezo vya asili vilivyopangwa katika Sehemu ya Kwanza ya Ratiba ya Kwanza inatumika katika utengenezaji wa bidhaa nyingine,

vigezo vya asili vitakavyoweza kutumika katika bidhaa hiyo, havitahusika navyo, na hakuna hesabu itakayofanywa kwa vifaa visivyo vya asili ambavyo vingetumika katika utengenezaji wake.

4. Endapo vigezo vya asili katika Sehemu ya Kwanza ya Ratiba ya Kwanza vinavyotumika kwenye bidhaa vitalingana na kufuata maudhui ya kiwango cha juu cha vifaa visivyo vya asili, ili viweze kulingana na kupanda na kushuka kwa bei na viwango vya sarafu, thamani ya vifaa visivyo vya asili na bei ya kazi za zamani zinaweza kukokotolewa kwa misingi ya wastani kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha tano.
5. Bei ya wastani ya kazi ya zamani ya bidhaa na thamani ya wastani ya vifaa visivyo vya asili vilivyotumika vitakokotolewa mtawalia kwa misingi ya:
 - a. Kujumlishwa kwa bei za kazi za zamani zinazolipishwa kwa mauzo yote ya bidhaa yaliyofanyika mwaka wa fedha uliopita; na
 - b. Kujumlishwa kwa thamani ya vifaa vyote visivyo vya asili vilivyotumika katika utengenezaji wa bidhaa kwa muda wa mwaka wa fedha uliopita kama ilivyoelezwa katika Nchi Mbia.
6. Iwapo hesabu ya mwaka wa fedha haipo kama inavyohitajika chini ya kifungu cha sita (6), kipindi kifupi cha muda usiopungua miezi mitatu kitatumika.
7. Mtengenezaji bidhaa au muuzaji bidhaa nchi za nje anayeamua kukokotoa thamani ya vifaa visivyo vya asili na bei ya kazi zamani kwa kutumia thamani ya wastani basi atatumia kila wakati njia hii wakati wa mwaka uliofuata mwaka wa fedha wa kumbukumbu, au ikibidi, wakati wa mwaka uliofuata kipindi kifupi kilichotumiwa kama kumbukumbu.
8. Mtengenezaji bidhaa au muuzaji bidhaa nchi za nje anaweza kuacha kutumia mbinu iliyotajwa katika kifungu cha tano (5) ambapo wakati wa mwaka wa fedha, au kipindi kifupi cha muda usiopungua miezi mitatu, iwapo mtengenezaji bidhaa au muuzaji bidhaa nchi za nje atarekodi kuwa kupanda na kushuka kwa gharama au viwango vya sarafu vilivyohalalisha kutumika kwa mbinu hiyo kumefikia kikomo.
9. Kwa ajili ya kuhakikisha utekelezaji wa Sehemu ya kwanza (1) ya Ratiba ya Kwanza, wastani wa bei ya kazi za zamani na thamani ya wastani ya vifaa visivyo vya asili mtawalia, itatumika.
10. Fauka ya Kifungu cha kwanza, vifaa visivyo vya asili ambavyo, kulingana na vigezo vya asili vilivyopangwa katika Sehemu ya Kwanza (1) ya Ratiba ya Kwanza havipaswi kutumika katika utengenezaji wa bidhaa fulani, vinaruhusiwa kutumika, iwapo jumla ya thamani au uzani wa neti wa bidhaa

hauzidi –

- (a) asilimia kumi na tano (15%) ya uzani wa bidhaa ambapo bidhaa ipo ndani ya Sura ya Pili (2) na ya Nne (4) hadi ya Ishirini na Nne (24) ya Mfumo Uliolingana; au
 - (b) asilimia kumi na tano (15%) ya bei ya kazi za zamani ya bidhaa, ya bidhaa nyingine, isipokuwa wakati ambapo bidhaa ipo ndani ya Sura ya 50 ha 63 ya Mfumo Uliolingana, ambavyo kwavyo, uvumilivu uliotajwa katika Sehemu ya Pili ya Ratiba ya Kwanza vitatumika.
11. Matumizi ya Kifungu cha kumi hayataruhusu yoyote kati ya asilimia za viwango vya upeo kwa vifaa maalum visivyo vya asili katika Sehemu ya Kwanza ya Ratiba ya Kwanza vizidishwe.
12. Mtengenezaji bidhaa au muuzaji bidhaa nchi za nje ataweka na kudumisha kumbukumbu ya gharama zote zitakazozingatiwa kwa ukokotozi wa bei ya kazi za zamani kulingana na Kanuni za Uhasibu Zinazokubalika kwa Ujumla zilizokubaliwa na Nchi Mbia ambapo bidhaa zinatengenezwa.

KANUNI YA SABA

Taratibu zisizoidhinisha asili/chimbuko

1. Mbali na Kanuni ya Sita, shughuli na michakato ifuatayo haitaidhinisha madai kuwa bidhaa zinatoka katika Nchi Mbia –
 - (a) Ufungaji, kuweka ndani ya chupa, chupa ombwe, mikoba na masanduku, kuweka kwenye kadi au mbao na shughuli nyingine rahisi za ufungaji;
 - (b) Uchanganyaji rahisi wa viungo vilivyonunuliwa kutoka nje ya hiyo Nchi Mbia;
 - (c) Uchangaji rahisi wa sehemu na vifaa vilivyonunuliwa kutoka nje ya Nchi Mbia, na kuunganishwa ili kutengeneza bidhaa kamili;
 - (d) Shughuli za kuhakikisha kuhifadhiwa kwa bidhaa katika hali nzuri wakati wa usafirishaji na kuhifadhi kama vile kwa kuingiza hewa safi, kueneza, kukausha, kugandisha, kuhifadhi kwa maji yaliyojaa chumvi, dioksidi ya sulfuri au maji yaliyo na mchanganyiko wa madini na uondoaji wa sehemu zilizoharibika na shughuli kama hizo;
 - (e) Kubadilika kwa ufungaji na uvunjaji au uunganishaji wa shehena;
 - (f) Kuashiria, kuweka alama au kuweka ishara za kuwezesha utofautishaji katika bidhaa au vifurusshi vyake;

- (g) Kazi rahisi ikiwemo utoaji vumbi, uchekechaji au uchunguzi, kuchagua, uainishaji au ulinganishaji, ikiwemo upangaji wa bidhaa, uoshaji, upanzi au kukatakata;
 - (h) upigaji pasi au mguruto wa nguo;
 - (i) Upakaji rangi rahisi au uchuaji rahisi;
 - (j) Utoaji makapi, upaushaji nusu au kwa ujumla, uchuaji, na matayarisho na nafaka na mpunga;
 - (k) Shughuli za kubadili rangi ya sukari au kutengeneza chembe chembe za sukari au usagaji wa sukari kwa ujumla
 - (l) Kumenya, kupiga mawe au utoaji maganda kwa matunda, njugu au mboga;
 - (m) Unojaji, kusaga au shughuli za ukataji; au
 - (n) Kuchinjwa kwa wanyama.
2. Kwa ajili ya Kanuni hii “rahisi,” kuhusiana na utengenezaji wa bidhaa inamaanisha mchakato ambao ujuzi wa kipekee, mashine, vifaa au zana zilizotengenezwa au kuwekwa kwa shughuli hizo hazihitajiki kwa mchakato huo.
 3. Shughuli zote zinazotekelezwa ndani ya Nchi Mbia kwa bidhaa fulani zitazingatiwa wakati wa kuthibitisha iwapo kazi hiyo au usindikaji uliopitiwa na bidhaa hiyo utachukuliwa kuwa haba kulingana na maana katika aya ya kwanza (1).

KANUNI YA NANE

Limbikizi la Asili

1. Bidhaa zinazotoka katika Nchi Mbia na ambazo zinapitia kazi au usindikaji katika Nchi Mbia nyingine, basi kwa ajili ya kuthibitisha asili ya bidhaa, itachukuliwa kuwa na asili ya mahali ilipofanyiwa kazi ya mwisho au mahali ulipofanyika usindikaji.
2. Bidhaa zinazotoka katika nchi au Ukanda wa Jumuiya ya Kiuchumi ambapo Jumuiya ya Afrika Mashariki imekamilisha Mkataba wa Eneo la Biashara Huria nayo, vitachukuliwa kuwa vifaa vilivyotoka ndani ya Nchi Mbia iwapo vifaa vitatengenezwa na kuwa bidhaa ndani ya hiyo Nchi Mbia, ambamo kazi au usindikaji uliofanyika ndani ya hiyo Nchi Mbia vitaenda zaidi ya shughuli zilizotajwa katika Kanuni ya Saba (7).

3. Vifaa vinavyotoka katika nchi au eneo linalofaidika na kutolipishwa kodi, lina fursa ya kufikia masoko bila upendeleo ya nchi au Ukanda wa Jumuiya ya Kiuchumi ambao Jumuiya imekamilisha Mkataba wa Eneo la Biashara nayo, zitachukuliwa kuwa vifaa vinavyotoka ndani ya Nchi Mbia iwapo vifaa vitatengenezwa na kuwa bidhaa ndani ya hiyo Nchi Mbia na usindikaji wa bidhaa hizo utaenda zaidi ya shughuli zilizotajwa katika Kanuni ya Saba.
4. Limbikizi iliotolewa katika aya ya tatu (3) haitatumika kwa vifaa vilivyo katika Ratiba ya Ushuru wa Pamoja wa Nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.
5. Bila upendeleo dhidi ya Kanuni ya Nne, vifaa visivyo vya asili ambavyo wakati wa uagizaji ndani ya Nchi Mbia kutoka kwa nchi ya kigeni, havipaswi kulipiwa ushuru wa forodha chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Ushuru wa Pamoja wa Nje, vitachukuliwa kuwa vifaa vilivyotoka ndani ya Nchi Mbia vitakapoingizwa na kuwa bidhaa zilitotengezwa ndani ya hiyo Nchi Mbia, ambamo vifaa vimepitia kazi ya kutosha au usindikaji zaidi ya ilivyotajwa katika Kanuni ya Saba (7).
6. Kanuni hii haitatumika kwa vifaa ambayo wakati wa uagizaji, vitakuwa chini ya Kanuni za Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Hatua za kupambana na ununuzi wa bidhaa duni) au Kanuni za Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Ruzuku na Hatua za Kupingana nazo).

KANUNI YA TISA

Kitengo cha Kufuzu

1. Katika uainishaji wa bidhaa chini ya Kanuni hii, kila bidhaa iliyo ndani ya shehena itazingatiwa kando.
2. Zaidi ya aya ya kwanza:
 - (a) ambapo Maelezo ya Bidhaa Yanayolingana na Mfumo wa Kuweka Alama vinataja kuwa kundi au mkusanyiko wa kifaa utaainishwa ndani ya kichwa kimoja, kundi kama hilo au mkusanyiko utachukuliwa kama kifaa kimoja; na
 - (b) vifaa, sehemu na vifuasi vilivyoagizwa pamoja na kifaa kimoja kutoka nchi za nje, ambavyo bei zake zipo pamoja na bei ya kifaa hicho au ambavyo kwavyo, hakuna ada zaidi iliyoitishwa, vitachukuliwa kuwa vya kuunda kifaa kizima, muradi vifaa na sehemu vinajumlika kutengeneza vifaaambavyo kwa kawaida huwekwa pamoja katika uuzaji wa kifaa aina hicho.

3. Kwa mifano ambayo haikutajwa katika aya ya pili, bidhaa zitachukuliwa kama kifaa kimoja kwa ajili ya kutathmini ushuru wa forodha kwa kifaa kama hicho kwa Nchi Mbia.
4. Kifaa ambacho hakijakusanywa au kilichootenganishwa, kinachoagizwa kwa shehena zaidi ya moja kwa sababu haiwezekani kwa minajili ya usafirishaji au utengenezaji kukiagiza kwa shehena moja, kitachukuliwa kama kifaa kimoja.

KANUNI YA KUMI

Mikusanyiko

1. Mkusanyiko, kama ulivyofafanuliwa katika Kanuni ya Tatu ya Utafsiri wa Ujumla katika Maelezo ya Bidhaa na Mfumo Maalum wa usimbuaji, uma inyiko ka tachukuliwa kama unaotoka katika Nchi Mbia iwapo sehemu zote za mkusanyiko huo zinatoka kutoka kwa hiyo Nchi Mbia.
2. Ambapo mkusanyiko unajumlisha bidhaa za asili na bidhaa zisizo za asili, mkusanyiko kwa ujumla utachukuliwa kuwa wa kutoka katika Nchi Mbia iwapo thamani ya bidhaa zisizo za asili haizidi asilimia kumi na tano (15%) ya bei ya kazi za zamani ya mkusanyiko huo.

KANUNI YA KUMI NA MOJA

Utengo wa Vifaa

Ambapo haiwezekani kwa mtengenezaji/mzalishaji kutenga vifaa vya aina moja lakini asili tofauti zilizotumika katika utengenezaji bidhaa, mtengezaji atatumia Kanuni za Uhasibu zinazokubalika kwa Ujumla zilizopitishwa na Nchi Mbia ambamo bidhaa inatengezwa, kuhakikisha hakuna bidhaa nyingine zinachukuliwa kutoka katika Nchi Mbia kinyume na itakavokuwa iwapo vifaa vingalitengwa.

KANUNI YA KUMI NA MBILI

Matayarisho ya Michanganyiko

1. Iwapo michanganyiko, ambayo si makundi au mikusanyiko ya bidhaa chini ya Kanuni ya tisa, Nchi Mbia inaweza kukataa kuikubali kuwa ya asili, bidhaa yoyote inayotokana na uchangaji wa bidhaa ambazo zinaweza kuhitimu kuwa na asili ya hiyo Nchi Mbia na bidhaa ambazo haziwezi kuhitimu kuwa na asili ya hiyo Nchi Mbia, ambapo sifa za bidhaa hiyo kwa ujumla hazina tofauti na sifa za bidhaa zilizochanganywa.
2. Kuhusu bidhaa fulani zinazotambulika na Baraza kuwa bora kuruhusiwa kuchanganywa kwa bidhaa zilizotajwa katika aya ya kwanza, bidhaa hizo zitakubaliwa kuwa na asili ya Nchi Mbia ikiwa sehemu ya bidhaa kama itakavyoonyeshwa kulingana na wingi wa bidhaa kutoka Nchi Mbia zinazotumika katika uchanganyaji na masharti yatategemea makubaliano ya Baraza.

KANUNI YA KUMI NA TATU

Matayarisho na Upakiaji

1. Kwa ajili ya kukadiria ushuru wa forodha, Nchi Mbia inaweza kutayarisha bidhaa kando na ufungaji na kwa ajili ya kuingiza bidhaa kutoka Nchi Mbia ingine, inaweza kuamua asili ya ufungaji ukiwa kivyake.
2. Ambapo aya ya kwanza haizingatiwi, ufungaji unaweza kuchukuliwa kutengeneza bidhaa kamili na hakuna sehemu ya ufungaji itakayohitajika katika usafirishaji au uhifadhi utachukuliwa kuagizwa kutoka nchi za nje ya Nchi Mbia katika kuamua asili ya bidhaa kwa ujumla.
3. Kwa ajili ya aya ya pili, ufungaji wa bidhaa ambazo kwa kawaida huuzwa kwa bei ya rejareja hautachukuliwa kama ufungaji unaohitajika katika usafirishaji au uhifadhi wa bidhaa.
4. Ambapo vifaa vya ufungaji na kontena ambazo bidhaa hupakiwa kwa uuzaji wa rejareja vitaainishwa pamoja na bidhaa kulingana na Kanuni ya Tano ya Utafsiri wa Ujumla katika Maelezo ya Bidhaa yaliounganishwa na mfumo maalum wa usimbuaji, vifaa vya ufungaji na kontena vitapuuzwa katika kuamua iwapo vifaa vyote visivyo vya asili vilivyotumika katika utengenezaji wa bidhaa ambapo

bidhaa hupitia mabadiliko yanayofaa katika uainishaji wa ushuru kama ilivyotakiwa katika Sehemu ya Kwanza ya Ratiba ya Kwanza.

5. Ambapo bidhaa zilizotajwa katika Aya ya Nne, zitahitaji thamani kuongezwa, thamani ya vifaa vya ufungaji na kontena vitazingatiwa kuwa vifaa vilivyo vya asili na vifaa visivyo vya asili, kama itakavyokuwa, katika kukokotoa thamani iliyoongezwa kwenye vidhaa.
6. Vifaa vinavyotumika tu katika usafirishaji au uhifadhi wa bidhaa kwa mda ambazo zitarudishwa, havitalipishwa ushuru wa forodha na malipo mengineyo.
7. Kontena zinazotumika katika usafirishaji au uhifadhi wa muda wa bidhaa, ambazo hazitarudishwa, zitatayarishwa kando na bidhaa zilizo ndani yake na zitalipishwa ushuru wa forodha na malipo mengineyo.

KANUNI YA KUMI NA NNE

Vipengele visivyohusika

Ili kuweza kuamua iwapo bidhaa inatoka ndani ya Nchi Mbia, haitakuwa lazima kuamua asili ya vitu vifuatavyo vinakotumika katika utengenezaji wake:

- (a) Nishati na Mafuta;
- (b) Viwanda na Vifaa;
- (c) Mashine na zana; na
- (d) Bidhaa zisizoingia na ambazo hazikusudiwi kuingia kwenye muundo wa mwisho wa bidhaa.

KANUNI YA KUMI NA TANO

Eneo

1. Isipokuwa kama ilivyoielezwa katika kanuni ya nane (8), bidhaa itafuzu kuwa iliyotoka ndani ya Nchi Mbia ambapo bidhaa hiyo itatimiza mahitaji ya kanuni ya nne (4) hadi kanuni ya kumi na nne (14).
2. Ambapo bidhaa za asili zilizosafirishwa kutoka kwa Nchi Mbia kwenda katika nchi ya kigeni

na kurudishwa katika Nchi Mbia, bidhaa hizo zitachukuliwa kuwa zisizo za asili, isipokuwa itakapoonyeshwa na kuridhisha Forodha kuwa:

- (a) Bidhaa hizo ni zilizokuwa zimesafirishwa hapo awali;
 - (b) Bidhaa hizo hazikupitia kazi iliyozidi kiwango kinachostahili kuzihifadhi katika hali nzuri zinapokuwa katika nchi ya kigeni au wakati zinaposafirishwa.
3. Hali ya asili iliyotolewa katika kanuni ya nne (4) hadi ya kumi na nne (14) haitaathiriwa na kazi au usindikaji uliofanywa nje ya Nchi Mbia kwa vifaa vilivyoagizwa kutoka hiyo Nchi Mbia na baadaye kurudishwa tena Nchini humo, ambamo:
- (a) vifaa hivyo vinapatikana ndani ya Nchi Mbia au kupitia kazi au usindikaji zaidi ya shughuli zilizotajwa katika kanuni ya saba (7) kabla ya kutolewa nje ya nchi; na
 - (b) inaweza kuonyeshwa na kuridhisha Forodha ya Nchi Mbia inayosafirisha bidhaa nje kuwa:
 - i. bidhaa zinazoagizwa nchini kwa mara ya pili zimepatikana kwa kufanya kazi au usindikaji wa bidhaa zilizokuwa zimesafirishwa nje; na
 - ii. thamani iliyopatikana nje ya Nchi Mbia kwa kutumia kanuni hii haitazidi asilimia kumi (10%) ya thamani ya forodha ya bidhaa ya mwisho ambayo kwayo hali ya asili inadaiwa na ambapo thamani hizo za forodha zitaamuliwa kulingana na masharti yaliyotolewa katika Kanuni za Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki za mwaka 2004.

KANUNI YA KUMI NA SITA

Usafiri wa Moja kwa Moja

1. Matayarisho ya Ushuru wa Jumuiya chini ya Makala ya Kumi na Nne ya Itifaki itatumika tu kwa bidhaa, ambazo baada ya kutimiza masharti ya kanuni hizi, zitasafirishwa kutoka kwa Nchi Mbia hadi nyingine.
2. Bidhaa zilizosafirishwa kuelekea nchi ya kigeni kwa ajili ya usafirishaji, ufungaji au michakato ambayo haitunuku hali ya asili haitostahikiwa chini ya Kanuni hii.

KANUNI YA KUMI NA SABA

Utoaji wa Cheti cha Asili

1. Msafirishaji anayedai kuwa bidhaa zinatoka kwa Nchi Mbia au mwakilishi aliyeidhinishwa na msafirishaji, atatoa maombi kwa kujaza fomu inayofaa kama ilivyoamrisha katika Ratiba ya Pili.
2. Ombi liliyofanywa chini ya aya ya kwanza litatakiwa kufuatwa na:
 - (a) ushahidi wa moja kwa moja wa michakato iliyofanywa na msafirishaji kupata bidhaa zinazohusika, zilizomo kwenye uhasibu au uwekaji vitabu wa msafirishaji;
 - (b) hati zinazothibitisha hali ya asili ya vifaa vilivyotumika, kulingana na sheria za kitaifa za hiyo Nchi Mbia;
 - (c) hati zinazothibitisha kazi au mchakato wa vifaa ndani ya Nchi Mbia ambamo hati hizi zitatumika kulingana na sharia za kitaifa za hiyo Nchi Mbia;
 - (d) cheti cha asili cha vifaa vilivyotumika, kilichotolewa na Nchi Mbia kulingana na kanuni hizi; na
 - (e) cheti kingine chochote kama itakavyohitajika na mamlaka yenye uwezo.
3. Ambapo msafirishaji si mtengenezaji/mzalishaji, msafirishaji huyo, kuhusiana na bidhaa zilizokusudiwa kusafirishwa, atatoa kwa mamlaka yenye uwezo, hati ya tamko rasmi kutoka kwa mtengenezaji inayoonyesha kuwa bidhaa zilitoka katika Nchi Mbia chini ya Kanuni ya Nne.
4. Tamko la mtengenezaji litakuwa katika fomu iliyotolewa katika Ratiba ya Tatu.
5. Mamlaka yenye uwezo ya Nchi Mbia itathibitisha maombi hayo na hali ya asili ya bidhaa, na itakuwa na haki ya kuitisha ushahidi mwingine wowote kuhusu hali ya asili na kutekeleza ukaguzi wa akaunti za msafirishaji au ukaguzi mwingine wowote utakaochukuliwa kuwa unafaa.
6. Mamlaka yenye uwezo ya Nchi Mbia, itakaporidhishwa na maombi na hali ya asili, itatoa cheti cha asili kwa msafirishaji kabla usafirishaji wenyewe haujatekelezwa.
7. Hata hivyo, zaidi ya yaliyoelezwa katika aya ya sita, mamlaka yenye uwezo ya Nchi Mbia, katika hali za kipekee, inaweza kutoa cheti cha asili baada ya usafirishaji wa bidhaa ambapo cheti kitakuwa na maelezo ya sababu zilizopelekea cheti hicho kutolewa.
8. Cheti cha asili kilichotolewa baada ya usafirishaji wa bidhaa kitaidhinishwa ndani ya Sanduku la Nne na msemu:

“ILİYOTOLEWA BAADA YA USAFIRISHAJI”

KANUNI YA KUMI NA NANE

Kutolewa kwa Nakala ya Cheti cha Asili

1. Katika tukio la wizi, kupotea au kuharibika kwa cheti cha asili, msafirishaji bidhaa anaweza kuiomba mamlaka yenye uwezo iliyotoa cheti hicho kumpa nakala.
2. Mamlaka yenye uwezo, kwa msingi wa maombi asili, itatoa nakala ya cheti cha asili.
3. Nakala ya cheti cha asili iliyotolewa chini ya aya ya pili itaidhinishwa ndani ya Sanduku la Nne (4) na msemu:

“NAKALA ya Cheti Nambari [.....] ya [Tarehe]”

4. Nakala ya cheti cha asili itaandikwa tarehe ya kutolewa kwa cheti asili cha asili na itakuwa halali kuanzia tarehe hiyo.

KANUNI YA KUMI NA TISA

Kutolewa kwa Cheti cha Asili kwa misingi ya ithibati ya asili ilitoyotolewa au kutengenezwa hapo awali

1. Ambapo msafirishaji angetaka kusambaza bidhaa za asili ndani ya Jumuiya, mamlaka yenye uwezo ambayo chini ya utawala wake bidhaa za asili huwekwa, inaweza kubadilisha cheti cha asili au tamko asili na cheti cha asili kama inavyohitajika.
2. Aya ya kwanza itatumika ambapo bidhaa za asili zitakuwa katika utawala wa forodha ya Nchi Mbia.
3. Cheti mbadala cha asili kinachotolewa chini ya kanuni hii kitaidhinishwa ndani ya Sanduku la Nne (4) na msemu:

“BADILISHO la [Nchi Mbia] Cheti Nambari [.....] cha [Tarehe]”

KANUNI YA ISHIRINI

Msafirishaji bidhaa nje aliyeidhinishwa

1. Msafirishaji bidhaa anayefanya usafirishaji wa mara kwa mara wa bidhaa chini ya kanuni hizi anaweza kuomba mamlaka yenye uwezo ya Nchi Mbia zinazofanya usafirishaji kuruhusiwa kuwa msafirishaji aliyeidhinishwa na kutoa maazimio ya asili.
2. Msafirishaji anayetoa maombi chini ya aya ya kwanza;
 - (a) atawasilisha nyaraka zilizotajwa katika kanuni ya 17(2); na
 - (b) atatoa dhamana muhimu kwa mamlaka yenye uwezo kuthibitisha hali ya asili ya bidhaa pamoja na ukamilishaji wa masharti mengine ya kanuni hizi.
3. Mamlaka yenye uwezo inaweza maombi ya msafirishaji chini ya aya ya kwanza kulingana na masharti ambayo mamlaka yenye uwezo itaona kuwa sahihi.
4. Mamlaka yenye uwezo itatoa nambari ya idhini kwa msafirishaji aliyeidhinishwa itakayoonekana katika tamko la asili.
5. Msafirishaji aliyeidhinishwa atatengeneza tamko la asili akitumia muundo uliotolewa katika Ratiba ya Nne.
6. Tamko la asili litakuwa na sahihi ya asili ya msafirishaji aliyeidhinishwa.
7. Tamko la asili linaweza kutengenezwa na msafirishaji aliyeidhinishwa wakati bidhaa zinazohusika nalo zinasafirishwa, au baada ya usafirishaji kwa sharti ya kuwa litawasilishwa kwa nchi inayoagiza mizigo kwa mda usiozidi miezi mitatu baada ya uagizaji wa bidhaa zinazohusika nayo.
8. Mamlaka iliyo na uwezo inaweza kubatilisha au kuondoa hali ya uuzaji bidhaa nje iliyoidhinishwa iwapo msafirishaji bidhaa –
 - (a) hatoi tena dhamana zilizotajwa katika aya ya kwanza nay a pili;
 - (b) hatimizi masharti yaliyotajwa katika aya ya tatu; au
 - (c) anafanya matumizi yasiyo sahihi ya idhini hiyo.
9. Mamlaka iliyo na uwezo, kupitia Sekretarieti, itafahamisha mamlaka ya Nchi mbia nyingine kuhusu wasafirishaji bidhaa walioidhinishwa na mamlaka hiyo.
10. Sekretarieti itadumisha hifadhidata ya wasafirishaji bidhaa walioidhinishwa kwa misingi ya habari iliyotolewa na mamlaka zilizo na uwezo za Nchi Mbia.

11. Mamlaka iliyo na uwezo itahakikisha kuwa data inayotumwa kwa Sekretarieti inafanyiwa marekebisho mara kwa mara, na iko kamili na sahihi.
12. Data inayodumishwa katika kanuni hii, isipokuwa habari ya siri kuhusu msafirishaji bidhaa aliyeidhinishwa, itakuwa wazi kwa umma.

KANUNI YA ISHIRINI NA MOJA

Uhalali wa ithibati ya asili

1. Cheti cha Asili kitakuwa halali kwa mda wa miezi sita kutoka siku iliyotolewa na mamlaka iliyo na uwezo ya Nchi Mbia inayofanya usafirishaji, na kuwasilishwa kwa Forodha ya Nchi Mbia iliyoagiza bidhaa ndani ya muda huo.
2. Tamko la asili litakuwa halali kwa muda wa miezi sita kutoka siku ya tamko na litawasilishwa ndani ya muda huo kwa Forodha ya Nchi Mbia inayoagiza bidhaa.
3. Forodha ya Nchi Mbia inayoagiza bidhaa inaweza kuruhusu cheti cha asili au tamko la asili vitakavyowasilishwa baada ya miezi sita katika mazingira ambayo Forodha imeridhika kuchelewa kwa kuwasilishwa kwa cheti cha asili au tamko la asili ilikuwa kwa ajili ya mazingira ya kipekee.
4. Cheti cha asili na tamko la asili vitawasilishwa kwa Forodha ya Nchi Mbia inayofanya uagizaji bidhaa kulingana na Sheria za Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2004.

KANUNI YA ISHIRINI NA MBILI

Kusamehewa kutoka kwa Cheti cha Asili

Bidhaa iliyotumwa kama kifurushi kidogo kutoka kwa mtu binafsi katika Nchi Mbia kuelekea kwa mtu binafsi katika Nchi Mbia nyingine, ambayo thamani yake haizidi Dola mia tano au inayotengeneza sehemu ya mzigo wa msafiri wa kibinafsi ambao thamani yake haizidi Dola elfu moja mia mbili, utakubaliwa kuwa bidhaa ya asili bila kuhitaji uwasilishaji wa uthibitisho wa asili, mradi bidhaa hiyo isiingizwe kwa njia ya biashara na imetangazwa kufikia mahitaji ya kanuni hizi na ambapo hakuna tashwishwi kuhusu ukweli wa tamko kama hilo.

KANUNI YA ISHIRINI NA TATU

Taarifa ya habari kuhusu mamlaka zenye nguvu

1. Nchi Mbia, kupitia Sekretarieti, itaarifu Nchi Mbia nyingine kuhusu –
 - (a) anwani ya mamlaka yenye nguvu ya hiyo Nchi Mbia; na
 - (b) maonyesho ya mfano wa mihuri mifano ya sahihi za maafisa walio dhinihwa kusaini vyeti.
2. Nchi Mbia zitaarifiana mara moja kila kutakapokuwa na mabadiliko kwenye habari iliyotajwa katika aya ya kwanza.

KANUNI YA ISHIRINI NA NNE

Uthibitishaji wa ithibati ya asili

1. Mamlaka iliyo na uwezo, katika hali ya kipekee na fauka ya uwasilishaji wa cheti cha asili kilichotolewa, au tamko la asili lililofanywa kulingana na kanuni hizi, itahitaji uhakiki zaidi wa habari iliyomo ndani ya cheti cha asili au tamko la asili.
2. Ambapo ombi la uhakiki zaidi linatolewa na mamlaka iliyo na uwezo chini ya kanuni hii, uhakiki utafanywa ndani ya miezi mitatu tangu kutolewa kwa ombi, kutumia fomu iliyotolewa katika Ratiba ya Tano.
3. Nchi Mbia inayoagiza bidhaa haitomzuia mwingizaji bidhaa nchini kupokea bidhaa kwa misingi ya kuwa inahitaji ushahidi zaidi tu, bali inaweza kuhitaji dhamana kwa ushuru au ada nyingine yoyote itakayohitajika kulipwa.
4. Forodha ya Nchi Mbia ambayo kwayo tamko la mtengenezaji linawasilishwa, inaweza kuomba Forodha ya Nchi Mbia ambamo tamko tamko lilitolewa kutoa cheti cha habari, kutumia muundo uliotolewa katika Ratiba ya Sita.

KANUNI YA ISHIRINI NA TANO

Uhifadhi wa hati

Hati zinazohitajika au kutolewa chini ya kanuni hizi zitaweka kwa mda wa angalau miaka mitano.

KANUNI YA ISHIRINI NA SITA

Ukiukaji na adhabu

1. Nchi Mbia ambayo kwayo madai ya uongo yanatolewa kuhusiana na asili ya bidhaa itaarifu Nchi Mbia inayosafirisha bidhaa mara moja ili kuweza kuchukuliwa hatua inayofaa.
2. Bila ubaguzi kwa aya ya kwanza, Nchi Mbia ambayo kwayo madai ya uongo yanatolewa kuhusu asili ya bidhaa, inaweza kutumia vifungu husika vya Sheria za Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2004.
3. Nchi Mbia ambayo, katika kufuatilia aya ya kwanza, imetaarifu Nchi Mbia inayofanya usafirishaji bidhaa kuhusu madai ya uongo, ambapo Nchi Mbia itaonelea bora kuwa hatua za kuridhisha hazijachukuliwa Nchi Mbia inayofanya usafirishaji kwa mda wa miezi mitatu inaweza kuwasilisha suala hilo kwa Kamati inayosimamia Suluhu za Kibiashara.
4. Ambapo suala limepelekwa kwa Kamati inayosimamia Suluhu za Kibiashara, Kamati hiyo itachukua hatua zinazofaa kulingana na vifungu husika kwa Mkataba huo.
5. Ukiukaji wowote utakaoendelezwa na Nchi Mbia dhidi ya masharti haya unaweza kupelekwa katika Baraza ambalo litachukua hatua kulingana na masharti ya Mkataba huo.

KANUNI YA ISHIRINI NA SABA

Mwongozo

Sekretarieti itaendeleza na kuhakiki miongozo kulingana na Kanuni hizi.

KANUNI YA ISHIRINI NA NANE

Maagizo kutoka kwa Baraza

Baraza litaweza kutoa maagizo kwa utekelezaji bora wa masharti ya kanuni hizi kulingana na makala ya kumi na nne ya Mkataba huo.

KANUNI YA ISHIRINI NA TISA

Kikomo cha Kanuni za Asili

Mkutano wa Kilele, baada ya mapendekezo kutoka kwa Baraza linalothibitisha kuwa malengo ya Umoja wa Forodha yamefanikiwa kikamilifu, utatangaza kukoma kwa kanuni hizi.

KANUNI YA THELATHINI

Kubatilishwa kwa Kanuni za Jumuiya ya Afrika Mashariki (Kanuni za Asili)

Kanuni za Umoja Wa Forodha Ya Jumuiya Ya Afrika Mashariki (Kanuni Za Asili) zilizoanza kutumika mnamo tarehe 1 Januari 2005 zimebatilishwa.

RATIBA YA KWANZA

ORODHA YA BIDHAHA NA KAZI AU SHUGHULI ZA USINDIKAJI ZINAZOJADILI ASILI

SEHEMU YA KWANZA

HS Nambari ya Kichwa	Maelezo ya Bidhaa	Vigezo vya Asili (Kazi au Shughuli za Usindikaji zinazofanywa juu ya bidhaa zisizo za asili zinazojadili hali ya asili)
Aya ya Kumi Aya ya Kumi na Moja	Nafaka. Bidhaa za tasnia ya kusaga; kimea; wanga; inulini; gundi ya ngano; isipokuwa kwa:	Utengenezaji ambamo vifaa vyote vya aya ya kumi vinavyotumika lazima vitengenezwe kabisa. Utengenezaji ambamo vifaa vyote vya aya ya kumi na kumi na kumi na moja, vichwa 07.01 na 23.03, na kichwa kidogo 0710.10 vinatengenezwa kabisa
Aya ya Ishirini na Tatu	Mabaki na taka kutoka kwa tasnia ya chakula; lische ya Wanyama iliyoandaliwa, isipokuwa kwa:	Utengenezaji bidhaa kutoka kwa vifaa vya kichwa chochote, isipokuwa vile vya bidhaa.
23.02 na 23.03	Kapi na mabaki mengine yatokanayo na kuchekecha, kusaga, au kazi nyingine za nafaka au za mimea ya kunde. Mabaki ya utengenezaji wanga.	Kutengeneza kutoka vifaa vya kichwa chochote, isipokuwa wa bidhaa, ambao uzani wa vifaa vya Aya ya kumi vilivyotumika hauzidi asilimia thelathini ya uzani wa bidhaa ya mwisho.
23.09	Matayarisho ya aina yanayotumika kulisha wanyama	Utengenezaji kutoka kwa vifaa vya kichwa chochote, isipokuwa ile ya kifaa ambacho kwacho:- vifaa vyote vya aya ya pili na ya tatu vinavyotumika vinatengenezwa kabisa, na Uzani wa vifaa vya Aya ya kumi na kumi na moja na vichwa 23.02 na 23.03 vinavyotumika havizidi asilimia 30 ya uzani wa bidhaa ya mwisho

SEHEMU YA PILI

Maelezo ya orodha katika Sehemu ya Kwanza

Kiandiko cha Kwanza: Utangulizi

- 1.1 Orodha inaweka wazi vigezo vya asili vinavyohitajika kwa bidhaa zote kuchukuliwa kuwa vimepitia kazi au usindikaji ndani ya maana ya kanuni ya sita ya kanuni hizi. Vigezo vifuatavyo vitatumika kama inavyostahili na ilivyoonyeshwa katika Sehemu ya Kwanza kwa heshima ya kila aya, kichwa au kichwa kidogo kama ilivyoielezwa katika safu ya kwanza:
- (i) kazi au usindikaji wa bidhaa fulani zilizotengenezwa kabisa;
 - (ii) kazi au usindikaji ambapo thamani ya vifaa vyote visivyo asili vinatumika kwa utengenezaji hauzidi kizingiti fulani cha juu;
 - (iii) kazi au usindikaji ambapo tarakimu nne za mfumo uliolingana kichwa au tarakimu sita za Mfumo Uliolingana kichwa kidogo mtawalia, ya vifaa vilivyotumika;
 - (iv) kazi maalum au usindikaji kazi inafanyika.
- 1.2 Vigezo vya asili vilivyotajwa hapo juu vinaweza kutumika bila kutegemeana au kama mbadala kama ilivyoielezwa katika Sehemu ya Kwanza.
- 1.3 Mifano: Matumizi ya Kiandiko 1.1 (ii)
- (a) ambapo kiwango cha juu cha vifaa visivyo asili vinavyotumika katika utengenezaji bidhaa hauzidi asilimia 70 ya bei ya kazi za zamani ya bidhaa iliyokamilika, inamaanisha thamani ya chini iliyoongezwa na mtengenezaji katika Nchi Mbia ni asilimia 30 ya bei ya kazi za zamani za bidhaa fulani.
 - (b) Ambapo bidhaa za vichwa 87.11 hadi 87.12, kiwango cha juu cha bei ya vifaa visivyo asili vilivyotumika katika utengenezaji havipiti asilimia 70 ya bei ya kazi za zamani ya bidhaa iliyokamilika, inamaanisha thamani ya chini iliyoongezwa na mtengenezaji katika Nchi Mbia ni asilimia 30 ya bei ya kazi za zamani za bidhaa hiyo.

Kiandiko cha Pili: Muundo wa Sehemu ya Kwanza

- 2.1 Safu mbili za kwanza katika orodha hiyo zinaeleza bidhaa iliyopatikana. Safu ya Kwanza inatoa nambari ya kichwa, kichwa kidogo au aya iliyotumika katika Mfumo Uliolingana na safu ya pili inatoa maelezo ya bidhaa zilizotumika kwenye mfumo huo kwa kichwa hicho, kichwa kidogo au aya. Kwa kila mjazo katika safu hizo mbili, kanuni zinaelezwa katika safu ya tatu. Ambapo, kwa nyakati fulani, mjazo katika safu ya kwanza unatangiwa na neno “ex,” hii inaonyesha kuwa kanuni zilizo katika safu ya tatu zinatumiwa tu kwa sehemu ya kichwa hicho au kichwa kidogo kama ilivyoelezwa katika safu ya pili.
- 2.2 Ambapo nambari za vichwa kadhaa au vichwa vidogo vinakusanywa pamoja kwenye safu ya kwanza au nambari ya aya kutolewa na maelezo ya bidhaa katika safu ya pili inatolewa kwa maneno ya jumla, kanuni zilizo kando katika safu ya tatu zitatumika kwa bidhaa zote ambazo, Chini ya Mfumo Uliolingana, zitaainishwa kwa vichwa vya aya au kwa yoyote kati ya vichwa vilivyokusanywa pamoja katika safu ya kwanza.
- 2.3 Ambapo kuna kanuni tofauti katika orodha zinazotumika kwa bidhaa tofauti katika kichwa, kila jongozo litakuwa na maelezo ya sehemu ya kichwa yaliyofunikwa na kanuni zilizo kando katika safu ya tatu.
- 2.4 Ambapo, kuweka mjazo katika safu mbili, zaidi ya kanuni moja inatajwa katika aya ya tatu, msafirishaji bidhaa anaweza kuamua, kama mbadala, kutumia yoyote kati ya kanuni zilizotajwa katika kanuni ya tatu.

Kiandiko cha Tatu: Mifaano ya jinsi kanuni zinavyotumika

- 3.1 Masharti ya kanuni ya sita ya Kanuni hizi kuhusu bidhaa zilizopata hali ya asili yanayotumika katika utengenezaji bidhaa nyingine yatumika hata ikiwa hali hii ilipatikana ndani ya kiwanda ambamo orodha ya bidhaa zilizotumika au katika kiwanda kingine katika Nchi Mbia.
- 3.2 Kufuatia kanuni ya saba, kazi au usindikaji uliofanyika lazima uzidi orodha ya kazi zilizotajwa katika kanuni hiyo. Isipofanya hivyo, bidhaa za mwisho hazitafuzu kupata matayarisho ya Ushuru wa Jumuiya, hata ikiwa masharti yaliyotolewa katika orodha ya Sehemu ya kwanza yanafuatwa.
- 3.3 Kanuni katika orodha zinawakilisha kiwango cha chini cha kazi au usindikaji unaohitajika na ufanyaji kazi au usindikaji wa ziada pia unatunuku hali ya asili; kinyume chake, kufanya kazi kidogo au usimbuaji hakuwezi kutunuku hali ya asili. Kwa hiyo kanuni inapoelekeza kuwa vifaa visivyo asili kwa kiwango fulani cha utengenezaji kitaweza kutumika, matumizi ya vifaa hivyo katika hatua ya awali ya utengenezaji yataruhusiwa na matumizi ya vifaa hivyo katika hatua ya awali ya utengenezaji utaruhusiwa na matumizi ya vifaa kama hivyo katika hatua ya baadaye hairuhusiwi
- 3.4 Bila ubaguzi dhidi ya Kiandiko cha 3.3 ambapo kanuni hutumia msemu “Kutengeneza bidhaa kutokana na vifaa vya kichwa chochote,” basi vifaa vya kichwa chochote (hata vifaa vya maelezo ya kichwa sawa sawa na bidhaa) vinaweza kutumika kulingana na mapungufu maalum yanayoweza kupatikana katika kanuni hiyo.

Hata hivyo, msemu “Tengeneza kutoka kwa vifaa vyenye kichwa chochote, pamoja na vifaa vingine vyilivyo na kichwa...” au “Tengeneza kutoka vifaa vyenye kichwa chochote vikiwemo vifaa vingine vilivyo na kichwa sawa na bidhaa” inamaanisha kuwa vifaa vya kichwa au vichwa vyovyote vinaweza kutumika, isipokuwa vile vilivyo na maelezo sawa na ya bidhaa kama ilivyotolewa katika safu ya pili ya orodha hiyo.


- 3.5 Ambapo kanuni iliyo kwenye orodha inataja kuwa lazima bidhaa itengenezwe kutoka kwa kifaa maalum, ni dhahiri kuwa sharti hilo halizuii matumizi ya vifaa vingine ambavyo kwa ajili ya asili ya asili, haiwezi kuridhisha kanuni hiyo.

Kiandiko cha Nne: Vifungu vya jumla vinavyohusu bidhaa Fulani za kilimo

Bidhaa za kilimo zinazoanguka chini ya aya ya 6, 7, 8, 10, 12 na kichwa 24.01 zinazovunwa ndani ya mipaka ya Nchi Mbia zitatarishwa kama zinazotoka ndani ya mipaka ya hiyo Nchi Mbia, hata zinapokuzwa kutokana na mbegu, vitunguu, kipande cha mzizi, vipandikizi, mashina au sehemu nyingine za mimea iliyo hai zilizoagizwa kutoka nchi ya kigeni.

RATIBA YA PILI

HATI YA UASILI WA BIDHAA YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

1. Msafirishi (Jina na Anwani ya ofisi)	Mfulizo Na.....: Kumb Na.....			
2. Mpelekewa (Jina na Anwani ya ofisi.)	 JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI			
3. Maelezo Kuhusu Usafiri utakaotumika	4. Kwa matumizi ya kiofisi tu			
5. Alama na Namba; namba na aina ya kifurushi, maelezo ya bidhaa	6. Na. ya ushuru wa Forodha	7. Kigezo cha uasili wa bidhaa	8. Uzito wa jumla au idadi nyingine	9. Namba ya Ankara Na tarehe
10. TAMKO LA MSAFIRISHAJI/ MZALISHAJI/ MGAVI Mimi Waliosainiwa hapa, wanatangaza kwamba maelezo hapo juu na taarifa ni sahihi, kwamba bidhaa zote zinazalishwa kwa (nchi) Mahali..... Tarehe..... Saini	11. UTHIBITISHO WA UASILI WA BIDHAA Inathibitishwa kuwa bidhaa zilizotajwa hapo juu zina asili ya Jina Sainiya Mamlaka Husika Tarehe..... Muhuri/Lakili			

Kanuni 17 (1)**MAELEZO KUHUSU KUJAZA HATI YA UASILI**

1. Msafirishaji lazima aingizwe kwenye fomu ya hati ya uasili taarifa inayohitajika katika kisanduku cha 1 hadi cha 10 fomu, isipokuwa kisanduku cha 4, ambacho kimewekwa kwa ajili ya matumizi ya ofisi.
2. Fomu inaweza kutayarishwa kwa mchakato wowote ili mradi maelezo yasifutike na yasomeke. Hairuhusiwi kufutafuta au kuongeza chochote katika fomu, na marekebisho lazima yafanywe kwa kukata maelezo yaliyokosewa na ndipo kuingiza nyongeza zinazohitajika. marekebisho ya aina hiyo lazima yawe na herufi za kwanza za jina la mtu aliyejaza fomu na kuidhinishwa na mamlaka au chombo kilichoteuliwa kutoa hati.
3. Nafasi yoyote katika fomu ambayo haijatumika ikatwe kwa mstari kwa namna ambayo itazuia kuongeza chochote.
4. Katika kisanduku cha 7 chenye kichwa cha habari” kigezo cha uasili wa bidhaa” kigezo maalumu kinachostahili chini ya kanuni ya 4 ya aya 1 ya jumuiya ya afrika masharaki ya uasili lazima kiingizwe. Kwa madhumuni haya, herufi zifuatazo lazima zitumike dhidi ya kila kipengelee kilichoingizwa kwenye fomu, kwa jinsi inavyofaa yaani:

“**P**” Kwa bidhaa ambazo kigezo cha uasili timilifu wa uzalishaji wa bidhaa kimetumika

“**M**” Kwa bidhaa ambazo kigezo cha matumizi ya malighafi ya ndani kimetumika.

“**C**” Kwa bidhaa zinazoainishwa kwa kigezo cha kubadilika kifungu cha utambulisho wa bidhaa katika tarakimu 4 au kifungu kidogo cha utambulisho wa bidha katika tarakimu 6 tofauti na utambulisho ule ilipoingilia kimetumika

“**S**” Kwa bidhaa ambazo kuna kiwango cha kazi mahususi au usindikaji umefanyika.


5. Taarifa ya msafirishaji ambayo inapaswa kutolewa katika kisanduku cha 10 ijumuishwe katika nafasi iliyowekwa, papo hapo kufuatia maneno “iliyozalishwa katika” nchi ambako bidha zimezalishwa.

6. Kabla ya kutia saini taarifa katika au kisanduku cha 11 ya fomu msafirishaji anapaswa kuhakikisha kuwa maelezo yote aliyoingiza kwenye fomu ni sahihi. Lazima awe tayari kutoa uthibitisho zaidi, ambao unaweza ukatakiwa na mamlaka ya uthibitisho kwa madhumuni ya kutoa hati, katika kisanduku cha 11 cha fomu.
7. Wakati msafirishaji ana uhuru wa kuamua ni nani atie saini kwenye taarifa kwa niaba yake, inafaa kwamba mtu aliyeidhinishwa kufanya hivyo awe ofisa wa kampuni ya msafirishaji. taarifa zinazotiwa saini na mawakala wa meli au wa usafirishaji au wengine kama hawa hazikubaliki.
8. Fomu ya hati ya uasili ijazwe katika nakala tatu kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye mamlaka yanayothibitisha.
9. Muhuri wa mamlaka yanayoidhinisha unapaswa kuwa na alama za kiusalama ambazo zinatambuliwa na jumuiya ya afrika mashariki.
10. Pamoja na matakwa ya sheria namba 19 na kwa kufuata utaratibu wa sheria namba 10 ni lazima mzigo uambatane na hati ya uasili wa bidhaa husika.

TANBIHI: Mtu yeyote ambaye kwa kufahamu anatoa au kusababisha hati ambazo si sahihi kutolewa katika jambo lolote hususan kwa madhumuni ya kupata hati ya uasili au wakati wa uthibitisho wa hati hizo, atakuwa na hatia, hivyo atastahili adhabu.

HATUA YA CHETI CHA AZILI YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

(Kwa bidhaa zenye thamani isiozidi US \$ 2000)

1. Msafirishi (Jina na Anwani ya ofisi)	Kumb Na	
	 JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI	
2. Mpelekewa (Jina na Anwani ya yakei)	3. Uthibitisho wa uasili wa bidhaa	
4. Maelezo ya bidhaa	5. Namba na aina ya kifurush	6. Thamani
<p>7. Tamko la Msafirishaji/Mzalishaji/Mgavi</p> <p>Mimi, Bwana / Bibi /Bi aliyepewa saina tangaza kuwa bidhaa zilizoelezwa hapo juu zimekuwa zinazozalishwa hi)..... kwa mujibu wa Kanuni za Asili za Jumuiya y' Afrika Mashariki.</p> <p>Saini</p> <p>Mahali</p> <p>Tarehe.....</p> <p>Muhuri.....</p>	<p>8. Uthibitisho wa forodha</p> <p>Mimi, aliyesainiwa hapa, ninakubali tamko la msafirishaji na ninathibitisha hilo bidhaa zinastahiki chini ya Kanuni za Asili z' Afrika ya Mashariki.</p> <p>Saini.....</p> <p>Mahali</p> <p>Tarehe.....</p> <p>Muhuri</p>	

RATIBA YA TATU

Tamko la Wauzaji/Watengenezaji bidhaa

A. Tamko la Wauzaji / Watengenezaji kwa bidhaa zilizo na hadhi ya asili

Mimi, aliyesainiwa chini, ninatangaza kuwa bidhaa zilizo rodheshwa kwenye namba ya Ankara hii

.....(1) zilitengenezwa mnamo (2) na kukidhi kanuni za asili zinazosimamia biashara kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Nchi Washirika au kati

Nchi Washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Ulaya au Nchi Wanachama wa FTA au Tatu kati ya Jumuiya ya Ulaya na nyingine nchi / kikundi cha nchi.....

Ninajitolea kutoa kwa mamlaka ya forodha, ikiwa inahitajika, ushahidi wa kuunga mkono tamko hili.

..... (3) (4)

..... (5)

Kumbuka

Nakala iliyotajwa hapo juu, iliyokamilishwa vyema kulingana na maelezo ya chini hapa chini, ni tamko la muuzaji. Manukuu hayalazimiki kuzalishwa tena.

(1) - Ikiwa tu bidhaa zilizo rodheshwa kwenye ankara zinahusika zinapaswa kuonyeshwa wazi au kuwekwa alama na uwekaji alama huu kwenye tamko kama ifuatavyo: “..... zilizo rodheshwa kwenye ankara hii na kuwekwa alama.....zilitengenezwa..... “

- Ikiwa hati isipokuwa ankara au kiambatisho cha ankara inatumiwa (angalia Kanuni ya 23 (4), jina la hati inayohusika litatajwa badala ya neno “ankara”.

(2) Jumuiya ya Washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, nchi au Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (RECs) ambazo Jumuiya ya Afrika Mashariki imehitimisha Eneo la Biashara Huria na au nchi zinazofaidika na upatikanaji wa soko la upendeleo.

(3) Mahali na tarehe

(4) Jina na kazi katika kampuni

(5) Saini

B. Tamko la Wamuuzaji / mtayarishaji wa bidhaa ambazo hazina hali halisi ya upendeleo

Mimi, aliyesainiwa chini, ninatangaza kuwa bidhaa zilizoordheshwa kwenye ankara hii (1)

zilitengenezwa mnamo (2) na ujumuishe yafuatayo

vifaa au vifaa ambavyo hazina asili ya Jimbo la Washirika wa Jumuiya ya Biashara ya upendeleo wa Jumuiya:

.....(3) (4).....(5)

..... (6)

Ninajitolea kutoa kwa mamlaka ya forodha, ikiwa inahitajika, ushahidi wa kuunga mkono tamko hili.

..... (7) (8)

..... (9)

Kumbuka

Nakala iliyotajwa hapo juu, iliyokamilishwa vyema kulingana na maelezo ya chini hapa chini, ni tamko la muuzaji. Manukuu hayalazimiki kuzalishwa tena.

(1) - Ikiwa tu bidhaa zilizoordheshwa kwenye ankara zinahusika zinapaswa kuonyeshwa wazi au kuwekwa alama na uwekaji alama huu kwenye

tamko kama ifuatavyo: “..... zilizoordheshwa kwenye ankara hii na kuweka alama zilitengenezwa “

- Ikiwa hati isipokuwa ankara au kiambatisho cha ankara inatumiwa (angalia Kanuni ya 28 (4), jina la hati husika litakuwa

zilizotajwa badala ya neno “ankara”

(2) Jimbo la Washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(3) Maelezo yanapaswa kutolewa katika hali zote. Maelezo lazima yatoshe na inapaswa kuwa na maelezo ya kutosha kuruhusu uainishaji wa ushuru wa

bidhaa zinazohusika ziamuliwe.

(4) Thamani za forodha zitolewe tu ikiwa inahitajika

(5) Nchi ya asili itolewe tu ikiwa inahitajika. Asili inayopaswa kupewa lazima iwe asili ya upendeleo, asili

zingine zote kutolewa kama “tatu nchi “.

(6) “na wamepitia usindikaji ufuatao katika Jumuiya la Washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki....., kwa kuongezwa na maelezo ya usindikaji unafanywa ikiwa habari hii inahitajika.

(7) Mahali na tarehe

(8) Jina na kazi katika kampuni

(9) Saini

RATIBA YA NNE**Kanuni 20 (5)****Tamko la uthibitisho wa Uasili**

Tamko la uthibitisho wa uasili kwa maelezo yote yaliyotolewa hapo chini, lazima yajazwe na msafirishaji:

“Msafirishaji wa bidhaa alietajwa katika fomu hii (Namba ya Usajili.....) anathibitisha kuwa bidhaa hizi

zimekidhi vigezo vya uasili wa bidhaa

.....

Mahali na Tarehe

.....

(Saini ya Msafirishaji, Pamoja na Jina Kamili la mtu anayesaini tamko hili)

RATIBA YA TANO

Kanuni 24(2)



FOMU YA UTHIBITISHO WA UASILI WA BIDHAA

SEHEMU A

Maelezo ya Bidhaa zinazohitaji Uthibitisho wa uasili

i. Namba ya Cheti[Lazima nakalla ya cheti iambatishwe]

ii. Mchakato/michakato ya uzalishaji inayofanywa

iii. Vifaa vilivyoingizwa kutoka nje Vinavyotengeneza na Nchi Wabia kutengeneza bidhaa zilizotajwa kwenye Hati, Thamani yake ya forodha na HS Codes

iv. Vifaa vinavyotoka jumuiya ya Africa Mashariki Vinavyotengeneza bidhaa zilizotajwa kwenye Hati, Thamani yake ya forodha na HS Codes

v. Makontena au aina nyingine ya ufungashaji wa ndani ambavyo kwa kawaida huuzwa pamoja na bidhaa kwa kiwango cha rejareja au vifaa vinavyotumika kuzitengeneza, thamani yake ya forodha ya asili na HS Codes

vi. Ushuru wa uingizaji bidhaa, kama upo unaolipwa kutokana na vifaa
vinavyoingizwa kutoka nje ya Nchi Wabi

vii. Gharama za kazi za moja kwa moja na za uendeshaji wa kiwanda

viii. Gharama za bidhaa zinazozalishwa nje ya kiwanda

ix. Gharama za ufungashaji wan je

x. Faida inayotokana na ongezeko la bei ya bidhaa zinazozalishwa

xi. Jumla ya bidhaa katika nchi zilikotengenezwa

Tamko

I

(Jina nna Cheo)

ya

(Jina la Kampuni)

.....

(Mahali)

.....

(Anuani)

Natamka kuwa maelezo na taarifa zilizotolewa hapo juu ni sahihi na kwamba zimetolewa kwa kuzingatia masharti ya sheria za uasili wa bidhaa.

PART B

Vyeti

Inathibitishwa kwa kuzingatia udhibiti uliofanywa kuwa tamko la Msafirishaji ni sahihi

.....

.....

.....

(Mahali na Tarehe)

.....

(Jina na Saini)

MUHURI

RATIBA YA SITA**Cheti cha habari cha Jumuiya ya Africa Mashariki**

1. Mzalishaji	CHETI CHA HABARI kuwezesha suala la UTHIBITISHO WA UASILI WA BIDHAA wa biashara iyayopendwa kati ya				
2. Mpelekewa (1)	<div style="border: 1px solid black; padding: 5px;"> NCHI WABIA YA JUMUIYA YA AFRICA YA MASHARIKI </div>				
3. Msindikaji (1)	4. Nchi ambayo kazi au usindikaji umefanywa				
6. Ofisi ya Forodha ya vifaa visivyo vya asili (1)	5. Kwa matumizi ya kiofisi				
7. Fomu ya kutoka (2) Fomu.....No..... Mfululizo Tarehe <table border="1" style="width: 100%; height: 20px;"> <tr> <td style="width: 33%;"></td> <td style="width: 33%;"></td> <td style="width: 33%;"></td> </tr> </table>					
VIFAA VINAVYOTOKA JUMUIYA YA AFRICA MASHARIKI					
8. Alama, idadi, wingi na aina ya kifurushi	9. Bidhaa chini ya kichwa au kichwa kidogo katika Maelezo ya Bidhaa yaliyounganishwa na mfumo maalum wa usimbuaji/ (code SH)	10. Kiasi (1) 11. Thamani (4)			

VIFAA VILIVYOINGIZWA KUTUMIKA

OMBI LA UTHIBITISHO	MATOKEO YA UTHIBITISHAJI
<p>Afisa wa forodha aliyesaini ombi uthibitisho wa ukweli na usahihi wa cheti hiki cha habari.</p> <hr/> <p style="text-align: center;">Mahali na Tarehe</p> <div style="border: 1px solid black; padding: 5px; width: fit-content; margin: 10px auto;">Muhuri wa ofisa</div> <hr/> <p>Sainiya Mamlaka Husika</p>	<p>Uthibitishaji uliofanywa na afisa wa forodha aliyesainiwa chini</p> <p>unaonyesha kuwa cheti hiki cha habari:</p> <p>a) ilitolewa na ofisi ya forodha iliyoonyeshwa na kwamba habari iliyomo ni sahihi (*)</p> <p>b) haitimizi mahitaji ya uhalisi na usahihi (angalia maelezo yaliyoongezwa (*))</p> <hr/> <p style="text-align: center;">Mahali na Tarehe</p> <div style="border: 1px solid black; padding: 5px; width: fit-content; margin: 10px auto;">Muhuri wa ofisa</div> <hr/> <p>Saini ya Mamlaka Husika</p> <p>(*) Futa pale ambapo haifai</p>

KUREJELEA

- (1) Jina la mtu binafsi au biashara na anwani kamili.
- (2) Habari ya hiari.
- (3) Kg, hl, m3 au kipimo kingine.
- (4) Ufungaji utazingatiwa kama kutengeneza jumla na bidhaa zilizomo humo. Walakini, kifungu hiki hakitatumika kwa vifungashio ambavyo sio vya aina ya kawaida ya nakala iliyojaa, na ambayo ina dhamana ya matumizi ya kudumu yake mbali na kazi yake kama ufungaji.
- (5) Thamani inapaswa kuonyeshwa kulingana na kanuni za asili.



East African Community

EAC Close
Afrika Mashariki Road
P.O. Box 1096
Arusha, Tanzania
Tel: +255 (0)27 216 2100
Fax: +255 (0)27 216 2190
Email: eac@eachq.org
www.eac.int

ISBN 978-9987-786-07-7



KANUSHO

Kitini hiki kimeweza kuandaliwa kwa msaada wa ukarimu kutoka kwa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Marekani (USAID). Yaliyomo kwenye kitini hiki yameandaliwa na Kituo cha kikanda cha Utafiti wa Maendeleo Jumuiishi (RCID Ltd) na hayalazimiki kuwa ni maoni ya USAID au Serikali ya Marekani.

